CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM
JUMUIYA YA WANATAALUMA (UDASA)
S.L.P. 35091 Dar es Salaam, Tanzania

**Baruapepe:** udasa@udsm.ac.tz **Tovuti:** udasa.udsm.ac.tz/

# TAMKO LA JUMUIYA YA WANATAALUMA WA CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM (UDASA) KUHUSU HALI YA KIUSALAMA NCHINI

Ndugu,

Watanzania Wote,

Mabibi na Mabwana,

UDASA ni Jumuiya Wanataaluma wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kama sehemu ya watanzania na tuliosomeshwa kwa kodi za watanzania tunao wajibu wa kufanya tafakari ya kina kuhusu kinachoendelea nchini na kutoa mapendekezo stahiki. Katika kutekeleza wajibu wetu huu, tutazungumzia mambo makuu mawili:

- Kutokuheshimu Haki za Watanzania
- Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025

## I. Kutokuheshimu Haki za Watanzania

Ibara ya 8(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaeleza kuwa, Tanzania ni nchi inayofuata misingi ya demokrasia na haki ya kijamii. Kwamba:

a) Wananchi ndio msingi wa mamlaka yote, na serikali inapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi;
b) Lengo kuu la serikali litakuwa ni ustawi wa wananchi; na,
c) Serikali itawajibika kwa wananchi.

Ibara ya 9 ya Katiba inazitaka mamlaka za nchi kuzingatia utu na kuhakikisha kuwa haki za binadamu zinaheshimiwa na kuthaminiwa. Mamlaka zinatakiwa kuhakikisha kwamba:

- Sheria za nchi zinalindwa na kutekelezwa;
- Heshima ya binadamu inahifadhiwa na kudumishwa kwa kufuata Kanuni za Tangazo la Dunia kuhusu Haki za Binadamu;



JUMUIYA YA WANATAALUMA
UDASA
23 OCT 2025
S.L.P 35091
DSM
CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

- Serikali na vyombo vyake vyote vinatoa nafasi zilizo sawa kwa raia wote, wake kwa waume, bila ya kujali rangi, kabila, dini au hali ya mtu;
- Aina zote za dhuluma, vitisho, ubaguzi, rushwa, na uonevu zinaondolewa nchini.

Ibara 13(4) inaeleza kuwa: ***ni marufuku kwa mtu yeyote kubaguliwa na mtu au mamlaka yoyote inayotekeleza madaraka yake chini ya sheria yoyote au katika utekelezaji wa kazi au shughuli yoyote ya Mamlaka ya Nchi***. Ibara ya 14(5) imetoa tafsiri ya neno 'kubagua' kuwa ni kutimiza haja kwa kupendelea makundi fulani kwa misingi ya kabila, mahali walipotokea, maoni yao ya kisiasa, rangi, dini, n.k. Inapotokea kiongozi au mamlaka fulani ikatangaza kuwa watu fulani watanyimwa huduma kwa sababu hawako upande fulani wa kisiasa, ni ubaguzi na ni kukiuka Katiba.

Ibara ya 13(6) (b) inaeleza: ***ni marufuku kwa mtu aliyeshtakiwa kwa kosa la jinai kutendewa kama mtu mwenye kosa hilo mpaka itakapothibitika kuwa anayo hatia ya kutenda kosa hilo***; na ibara ya 13(6)(e) inasema kuwa, ***ni marufuku kwa mtu kuteswa, kuadhibiwa kinyama au kupewa adhabu zinazomtweza au kumdhalilisha***.

Tumerejea ibara hizi kama kutoa msingi wa hoja zetu kuhusu utekaji na aina nyingine za ukatili zinazofanywa na vyombo vya dola dhidi ya raia. Kwa sasa, **watu wasiojulikana** wamekuwa juu ya katiba na siyo watu wanaoguswa wala kudhibitiwa. Matendo yao ya kikatili yanakiuka ibara ya 13(6)(e) iliyorejewa hapo juu.

Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita tumeshuhudia ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu na ukiukwaji wa Katiba. Taarifa rasmi za Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), na Shirika la Amnesty International, ambazo ni taasisi zinazotambulika kwa kufanya tafiti na utetezi wa haki za binadamu nchini na kimataifa, zimeonyesha kuwa, katika nchi yetu, kuna ukikukwaji mkubwa wa haki za binadamu na ukiukwaji wa Katiba sheria nyinginezo.

Katiba ya Tanzania inaeleza kuwa Serikali na vyombo vyake vitakuwa na wajibu wa kutoa nafasi sawa kwa raia wote na kuhakikisha vitendo kama vile dhuluma, vitisho, ubaguzi,



JUMUIYA YA WANATAALUMA
UDASA
23 OCT 2025
S.L.P 35091
DSM
CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

rushwa, na uonevu kwa raia wake vinadhibitiwa. Kwa bahati mbaya masuala ya utekaji, mauaji, na kupiga watu kinyama yamekuwa ya kawaida kwa miaka ya hivi karibuni. Je serikali na vyombo vyake vya dola wameshindwa kuyadhibiti kikamilifu matukio haya na hivyo kushindwa kutekeleza wajibu wake wa kikatiba?

Mbali na matatizo mengi ya ukiukwaji wa haki za binadamu, UDASA tungependa kujielekeza zaidi katika masuala machache:

i. Utekaji na watu kupotea na kutojulikana walipo;
ii. Watuhumiwa wa makosa mbalimbali kukamatwa kinyume cha sheria na kuwekwa kizuizini bila ya kufunguliwa mashtaka;
iii. Wananchi na vyama vya upinzani kunyimwa haki sawa katika kushiriki kwenye mchakato wa kidemokrasia nchini;
iv. Kusuasua kwa utekelezwaji wa mapendekezo ya Tume ya Rais ya Haki Jinai ya 2023 katika usimamizi wa haki. Kuhusiana na hili, ni vema kukawa na utashi wa kisiasa wa kuyafanyia kazi mapendekezo ya Tume hii ili watanzania wawe na imani na mifumo ya kutoa haki nchini.

Kwa mujibu wa ripoti ya haki za binadamu LHRC, kumekuwa na tishio kubwa na jipya nchini linaloitwa **"watu wasiojulikana"** walioibuka na kuwa kikundi cha watu hatari zaidi nchini kutokana na jeshi la Polisi ama kushindwa kulidhibiti au kushindwa kutolea ufafanuzi wa matukio yanayohusisha kundi hilo. Bahati mbaya zaidi ni kwamba, wasiojulikana wamekuwa juu ya sheria na utawala wa sheria hauna nafasi tena kwani wanaoangukia mikononi mwa kundi hilo wanapotea.

Kwa ujumla, LHRC wanabainisha kuwa **kati ya mwaka 2020 na 2024, kulikuwa na matukio 87 ya watu kutekwa na kupotezwa**. Ripoti ya LHRC inaonyesha kuwa matukio 31 yalitokea mwaka 2022 na matukio 33 mwaka 2024. Mbali na watu waliotekwa na kupotea kwa kipindi hicho, ripoti hiyo imeonyesha kuwa kati ya mwaka 2020 na 2024, watanzania waliouawa kinyume cha sheria na vyombo vya usalama kama vile Jeshi la Polisi na Askari wa Wanyamapori (Jeshi Usu), walifikia 36. Jedwali hapa chini linatupa muhtasari wa matukio ya watu kutekwa, kupotezwa na kuuawa kinyume cha sheria.



JUMUIYA YA WANATAALUMA
UDASA
23 OCT 2025
S.L.P 35091
DSM
CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

Jedwali kuonesha Idadi ya matukio ya utekaji na mauaji kuanzia mwaka 2020-2024

| Mwaka | Idadi ya matukio ya utekaji na kupotezwa kwa wananchi | Asilimia (%) | Matukio ya mauaji ya raia yaliyofanywa na vyombo vya usalama (%) | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|
| 2020 | - | - | 4 | 11.11 |
| 2021 | 11 | 12.64 | 9 | 25.00 |
| 2022 | 31 | 35.63 | 10 | 27.78 |
| 2023 | 12 | 13.79 | 7 | 19.44 |
| 2024 | 33 | 37.93 | 6 | 16.67 |
| **Jumla** | **87** | **100** | **36** | **100** |

Hii inaonyesha kuwa watanzania wanaokuwa mikononi mwa vyombo vya usalama wa raia hawana uhakika wa kuwa salama kutokana na matumizi ya nguvu za kupita kiasi na vyombo hivyo kutotumia weledi katika kushughulika na watuhumiwa wa uhalifu. Ikumbukwe kuwa sheria zetu zinaeleza kuwa mtu anabaki kuwa mtuhumiwa tu hadi Mahakama itakapothibitisha kuwa ana hatia.

Ukosefu huu wa weledi kwa upande wa vyombo vya usalama wa raia kama vile Jeshi la Polisi kutawafanya watanzania wakose imani na jeshi lao (na kimsingi tayari kuna viashiria vya kukosa imani hii) na hivyo kujichukulia sheria mkononi kwa ajili ya kujihami na vitendo vya ukiukwaji wa sheria vinavyofanywa **na watu wasiojulikana ambao Polisi wameshindwa kuwadhibiti**.

Tukumbuke tukio la Desemba mwaka 2024 lililotokea Tegeta, Dar es Salaam ambapo Afisa wa Mamlaka ya Mapato (TRA), Ndugu Amani Simbayai, aliuawa na wananchi wenye hasira wakimfananisha na watekaji (watu wasiojulikana). Ilithibitika baadaye kuwa alikuwa kwenye majukumu yake ya kikazi na hakuwa na nia ya kumdhuru yeyote.

Turejeshe kumbukumbu zetu pia kwenye lile tukio la mwaka 2016 ambapo watafiti Teddy Lumanga na Jaffari Mafuru na dereva wao Nicas Magazine wa Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha Selian (SARI) cha Mkoani Arusha waliouawa na miili yao kuchomwa moto katika kijiji



JUMUIYA YA WANATAALUMA UDASA 23 OCT 2025 S.L.P 35091 DSM CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

cha Iringa-Mvumi wilayani Chamwino mkoani Dodoma wakati wakifanya utafiti wa udongo, baada ya kuhisiwa kuwa ni wanyonya damu.

Matukio haya yanaonyesha kuwa wakati mwingine, wananchi wakikosa imani na Taasisi za Serikali na Vyombo vya Ulinzi na Usalama kama vile Jeshi la Polisi, watawaona maofisa wa serikali kuwa maadui wao. Madhara yatakuwa makubwa kwani wananchi wa kawaida hawataweza kuwatenganisha wafanyakazi walioko kwenye majukumu yao ya kawaida na wale wanaoweza kuwadhuru (watekaji). Watajichukulia sheria mkononi ya kuamua kujihami, na hivyo utulivu nchini kukosekana.

Lakini pia tujikumbushe tukio la kuuawa kwa Bwana George Juma Mohamed na Polisi wakati wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka jana 2024 kule Manyoni Singida. Tusisahau pia kupotea kwa Shadrack Chaula aliyeonekana akichoma picha ya Rais Samia. Ndugu Shadrack alikamatwa na watu wasiojulikana mwezi Agosti mwaka 2024 kule Mbeya. Hata kama kitendo chake cha kuchoma picha ya Rais Samia lilikuwa kosa, hakustahili kutekwa na kupotezwa. Kisheria, ilitakiwa ashitakiwe na kuhukumiwa kisheria, kwani huo ndio utawala wa sheria na ndiyo namna bora ya vyombo vya dola kuheshimu Katiba, sheria, kanuni na taratibu za nchi.

Utekwaji na kupotezwa kwa watanzania wenzetu kumeonekana kubeba taswira ya chuki za kisiasa, na vikosi hivi vya watekaji vinawalenga zaidi wakosoaji wa serikali na Rais Samia. Jambo hili halileti taswira nzuri kwa nchi yetu kwani linaharibu maana na mantiki nzima ya kuwa na demokrasia ya vyama vingi na utawala bora.

Chuki hizi dhidi ya wakosoaji wa Rais na kuwalenga vyama vya upinzani zinadhihirika kwa kutekwa na kupotea kwa vijana Deusdedith Soka, Jacob Mlay na Frank Mbise waliokamatwa tarehe 18 Agosti 2024 kule Buza, Dar es Salaam na haijulikani waliko hadi leo. Vile vile, mkosoaji mwingine wa Rais Samia na Serikali yake, Mdude Nyagali naye alikamatwa akiwa nyumbani kwake na kupelekwa kusikojulikana mpaka leo.



JUMUIYA YA WANATAALUMA UDASA 23 OCT 2025 S.L.P 35091 DSM CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

Mwezi Septemba mwaka 2024 taifa letu lilihuzunishwa kwa taarifa za kutekwa na kuuawa kwa Bwana Ali Kibao aliyekuwa kiongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA). Mauaji yale yalikuwa ya kikatili sana na yaliamsha hisia nyingi miongoni mwa watanzania kuhusu usalama wao kwani watekaji wamekuwa si waoga tena hadi wanaweza kumshusha mtu kwenye basi na kumfanyia ukatili ule. Hisia kama hizo zimeamshwa tena tarehe 6 Oktoba 2025 baada ya kutolewa taarifa za kutekwa kwa Ndugu Humphrey Polepole na kupelekwa kusikojulikana mpaka leo.

Uwepo wa vikosi vya watu wasiojulikana wanaohusika na masuala ya utekaji nchini una athari nyingi kwa ustawi wa taifa letu. Ni jambo la lazima na muhimu kwa vyombo vya usalama kukomesha vikosi hivi kwa haraka, kwani bila ya kufanya hivyo, usalama wa watanzania utazidi kuwa hatarini. Hofu yetu inatokana na uwezekano wa kutokea kwa hatari zifuatazo:

1. Tutakuwa na taifa la watu waoga ambao watashindwa kuwa wabunifu na kutoa mchango kwa ajili ya ujenzi wa taifa. Watanzania wenye vipaji vya ubunifu kama vile sanaa, fasihi, utunzi wa nyimbo, na uandishi wataogopa kuonya, kukosoa na hata kuelimisha kupitia kazi zao kwa hofu ya kupotezwa/kutekwa.

2. Ipo hatari ya kuwafanya watanzania waichukie serikali na nchi yao kwa sababu ya kuona matukio ya kikatili yanatawala maisha yao ya kila siku. Hali hii inaweza kutoa nafasi kwa maadui wa nje kushirikiana na maadui wa ndani kufanya jambo/mambo mabaya kwa nchi yetu na raia wake.

3. Kama vikosi vya watekaji vitatumika kama njia ya kuwanyamazisha na kuwadhibiti wakosoaji wa Rais na Serikali, basi watekaji hao wanaweza kujikita mizizi kwenye mifumo yote ya kiutawala na baadaye kutumika na viongozi wa Wizara, Idara, Taasisi na Wakala za serikali kuwateka wakosoaji ambao wataonekana mwiba kwao. Tusipodhibiti hili tutajikuta wakosoaji wa Mawaziri wanatekwa kwa sababu wataona ndiyo njia rahisi ya kuwadhibiti wakosoaji wao. Itawezekana pia sisi wahadhiri wa Chuo Kikuu pia kutengeneza magenge ya kuwateka wanaosema ubora wa elimu tunayoitoa umeshuka. Tusiruhusu



JUMUIYA YA WANATAALUMA
UDASA
23 OCT 2025
S.L.P 35091
DSM
CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

utekaji iwe ni njia ya kuwaadhibu wanawakosoa viongozi wa aina yoyote ile.

4. Kitendo cha mamlaka za juu za nchi kutochukulia utekaji na kupotea kwa watu kwa upekee wake kutafanya suala hili kuwa gumu na kushindwa kung'amua mapema viashiria vya kuibuka kwa makundi ya kigaidi. Ipo hatari ya wananchi na Jeshi la Polisi kuendelea kupuuzia hata matukio yenye viashiria vya ugaidi na matokeo yake ugaidi utashamiri na kusambaa na kuja kuwa tatizo kubwa. Tukumbuke "Usipoziba Ufa, Utajenga Ukuta", na "Kinga ni Bora Kuliko Tiba."

5. Matukio kama lile la Oktoba 16, 2025 la vijana wanne wa Tabata/Vingunguti (Dar es Salaam) kupotea na kisha miili yao kuokotwa kule Kibaha ni dalili mojawapo inayotupa ishara kuwa tatizo hili la utekaji linaweza kuwa na sura nyingi. Kuna matukio ya utekaji yanayoweza kufanyika kwa sababu ya ugomvi wa kifamilia, ugomvi wa mahusiano, kudhulumiana kwenye biashara, kafara za biashara, ushirikina, visasi kwenye jamii na hata chuki za kisiasa. Ni jukumu la vyombo vyetu vya usalama kuyafuatilia matukio haya na kuyakomesha mara moja. Ni wajibu wa dola pia kutoa taarifa juu ya matukio haya na kuchukua hatua stahiki kwa wahusika wote.

6. Kutokana na mwenendo wa kisiasa unaoendelea nchini, tumeanza kuona chuki za kisiasa zikiongezeka na kusambaa kwa kasi. Kama vyombo vyetu vya usalama havitaweza kulikomesha tatizo hili la utekaji na watu kupotezwa, kuna uwezekano mkubwa wa utekaji kuongezeka. Na hili lisidhaniwe kuwa kati ya Upinzani na Chama Tawala, bali hata ndani ya Chama Tawala na Upinzani pia wakadhuliana wao kwa wao.

Hivyo ni muhimu sana kuchukua hatua za haraka kukomesha tatizo hili la utekaji kwa ajili ya ustawi wa vizazi vya sasa na baadaye. Tusiruhusu siasa kuwa chanzo cha uadui kwa watanzania kwani Katiba ya nchi yetu inatamka wazi kuwa nchi yetu ni ya demokrasia ya vyama vingi.



JUMUIYA YA WANATAALUMA
UDASA
23 OCT 2025
S.L.P 35091
DSM
CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

Wananchi wawe huru kushiriki kwenye siasa na kuikosoa serikali na viongozi wake ilimradi hawavunji Katiba na sheria za nchi. Wananchi wasiogope kukosoana kwenye siasa na kuwakosoa viongozi wao kwa sababu ya vikosi hivi vya utekaji. Ikumbukwe kuwa Katiba inaeleza kuwa madaraka ya serikali yanatoka kwa wananchi. Umuhimu wa wananchi usiwe tu wakati wa uchaguzi bali liwe ni jukumu la kudumu kwa serikali kuwajali, kuwalinda, kusikiliza hoja zao (hata kama hawazipendi) na kuwaheshimu.

## II. Hali ya Kuelekea Uchaguzi Mkuu Tarehe 29 Oktoba 2025

Tunapoelekea siku ya Uchaguzi Mkuu tarehe 29 Oktoba, tumeshuhudia makundi makuu mawili ya watanzania. Wapo wanaofanya kampeni ya kupiga kura siku hiyo (Oktoba Tunatiki) na kundi jingine linawahimiza watanzania wasiende kupiga kura na badala yake waandamane (Oktoba Tunatoka). UDASA tunaamini kuwa kupiga kura ni wajibu wa kila mtanzania na ni haki ya kila mtanzania kuchaguliwa kuwa kiongozi wa nchi hii kama ambavyo Katiba na sheria zetu zinavyotuelekeza.

Hali hii imetokana na namna mchakato mzima wa maandalizi na usimamizi wa uchaguzi yanavyofanyika. Toka awali, kama taifa hatukujielekeza katika kutafuta mwafaka wa kitaifa kwa kuwahusisha wadau wote kuufanya uchaguzi huu mkuu uwe shirikishi. Tungependa kuzisihi pande zote zinazovutana zijiepushe na kuchochea vurugu. Tukubali kuwa kuna mahali tulifanya makosa ili tujisahihishe.

Hivyo tungependekeza masuala yafuatayo yafanyike mapema iwezekanavyo baada ya uchaguzi kwa ajili ya kuliponya taifa na majeraha yaliyojitokeza.

a. Wanasiasa wasijione wao pekee ndio wenye haki zote kuhusu michakato ya kidemokrasia nchini. Haki ya kuchagua na kuchaguliwa ni ya watanzania wote na uamuzi wa mustakabali wa kisiasa uwe mikononi mwa watanzania.

b. Bunge lijalo litambue kuwa lenyewe ni muhimili unaojitegemea na liko kwa ajili ya maslahi ya wananchi. Linapaswa kuwa na wivu mkuu juu ya hadhi na uhuru wake. Itafaa kama wabunge watatunga sheria ya kuwakinga raia dhidi ya nguvu za vyama wanapogombea nafasi mbalimbali za uongozi.



JUMUIYA YA WANATAALUMA
UDASA
23 OCT 2025
S.L.P 35091
DSM
CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

c. Vyombo vya ulinzi na usalama na taasisi za dola zijiepushe kutumika kisiasa. Badala yake, wajielekeze katika msingi wa majukumu ya kuilinda na kuitetea Katiba ya Tanzania na kuwahudumia watanzania wote. Kitendo cha vyombo hivi vya dola kuwa upande wa Chama Tawala kinaondoa imani kwa wananchi na ni kinyume cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Matokeo ya kuchagua kuwa upande wa Chama Tawala badala ya kutenda haki kwa kila raia ni kutengeneza chuki baina ya makundi mbalimbali ya watanzania.

d. Viongozi wetu wa kisiasa wenye kinga za kisheria wajiepushe na kauli tata wanapokuwa majukwaani kwani wana jukumu kubwa la kuwanganisha watanzania wote hasa kipindi hiki ambapo mshikamano na umoja wa kitaifa umeporomoka sana. Tunawategemea viongozi wetu wa kitaifa kuliokoa taifa na kuepuka kutoa kauli zinazotonesha majeraha ya kukandamizwa na kuonewa kwa kutumia dola na vyombo vingine vya usalama.

e. Ni muhimu kwa viongozi wetu walio na kinga ya kisheria kujizuia kudharau Katiba. Labda tuwe na mabadiliko huko mbeleni lakini kwa sasa, Katiba ndiyo sheria mama au sheria namba moja ambayo kila mtanzania lazima aheshimu na kuifuata. Siyo busara kwa viongozi walioapa kuilinda Katiba waivunje. Pasiwepo na kiongozi yeyote anayeweza kudharau Katiba na kuwa juu ya sheria. Watanzania tusimame imara na kumwambia HII HAIKUBALIKI.

f. Kuundwe Tume ya Kijaji au Kamati Maalum ya Bunge ambayo itachunguza matukio ya utekaji na upoteaji wa watu ili haki itendeke kwa waliofanyiwa matendo hayo. Tume hiyo ya Kijaji au Kamati ya Bunge itabainisha kiini cha tatizo na kutoa mapendekezo ili hatua stahiki zichukuliwe kukomesha vitendo hivi. Hata kama utekelezaji wa mapendekezo hayo utahitaji utashi wa kisiasa, ripoti ya tume hiyo itaweza kuwafariji waathiriwa wa matendo hayo.



JUMUIYA YA WANATAALUMA
UDASA
23 OCT 2025
S.L.P 35091
DSM
CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

Baada ya Uchaguzi Mkuu, tunakitaka Chama chochote kitakachoshika madaraka kuanzisha mchakato wa maridhiano ya kitaifa utakaotokana na utashi wa kisiasa. Masuala yafuatayo yapewe kipaumbele kwenye mchakato huo wa maridhiano:

- Tume Huru ya Uchaguzi iwe na uwakilishi wa makundi yote ya kisiasa, kijamii, kidini, na asasi za kiraia. Wajumbe wakishapatikana wao ndiyo wamchague Mwenyekiti wa Tume atakayeapishwa na Jaji Mkuu badala ya kuteuliwa na Rais ambaye naye pia ni mgombea wa uchaguzi.

- Makosa yanayohusiana na uchaguzi yasichukuliwe kama makosa ya jinai badala yake yawe ya kusahihishwa na kutoa nafasi kwa wadau wa kisiasa kuyarekebisha bila ya kuwanyima wahusika haki ya kushiriki kwenye mchakato wa uchaguzi.

- Vyombo vya habari visinyimwe uhuru wa kutoa taarifa zinazohusu kasoro za uchaguzi wanazoziona kwa ushahidi wa wazi. Pia vyombo vya habari viruhusiwe kuwa sehemu ya kupigania na kusimamia uwazi katika mchakato wa uchaguzi na kama kuna mapungufu visaidie kuyaibua na mamlaka husika ziweze kuyarekebisha.

- Vyombo vya usimamizi wa sheria kama vile Jeshi la Polisi vijiepushe na matumizi makubwa ya nguvu wakati wa kampeni na kupiga kura. Vitendo vyao vinawafanya watanzania waogope kushiriki katika kampeni na pia kupiga kura.

- Ni muhimu kuhakikisha kuwa kuna uwazi wakati wa kuandikisha wapiga kura, kwenye daftari la wapiga kura na hata wakati wa kuhesabu na kujumlisha kura ili zoezi zima la uchaguzi liwe la kuaminika kwa watanzania na kuuonyesha ulimwengu kuwa michakato yetu ya uchaguzi ni ya kidemokrasia. Tuache ujanja ujanja ambao unaidhalilisha na kuifedhehesha nchi yetu.



JUMUIYA YA WANATAALUMA
UDASA
23 OCT 2025
S.L.P 35091
DSM
CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

UDASA tunasisitiza kuwa watanzania wana haki ya kuishi kwa amani katika nchi yao. Wana haki ya kuendesha shughuli zao bila ya kubaguliwa kisiasa. Tunavisihi vyombo vya dola na taasisi za haki nchini kuheshimu Katiba na sheria za nchi yetu.

Ibara ya 17(1) inaeleza kuwa: ***Kila raia wa Jamhuri ya Muungano anayo haki ya kwenda kokote katika Jamhuri ya Muungano na kuishi katika sehemu yoyote, kutoka nje ya nchi na kuingia, na pia haki ya kutoshurutishwa kuhama au kufukuzwa kutoka katika Jamhuri ya Muungano.*** Hivyo, ni muhimu kutambua kuwa hakuna anayeweza kuwa juu ya Katiba na sheria ambayo mamlaka zetu zinaapa kuzilinda. Kama walinzi na wasimamizi wa Katiba na Sheria wanaanza kukiuka matakwa ya nyenzo hizi, watanzania watakimbilia wapi?

Ni vema kuelewa kuwa Tanzania siyo kisiwa. Tujifunze kupitia methali ya Kiswahili kuwa **Mwenzako Akinyolewa, Zako Tia Maji**. Ulimwengu wetu ni wa kidijitali. Tuliyoyashuhudia yakitokea katika nchi nyingine huko duniani, na tena baadhi zikiwa nchi rafiki na majirani zetu, sisi hatuna kinga. Kwa mfano, tumeshuhuhudia machafuko ya kisiasa katika nchi za Nepali na Mdagascar. Katika nchi hizo tumeona viongozi waliotumia vyombo vya ulinzi na usalama kuwakandamiza wananchi na wapinzani namna walivoondoshwa.

Itafika wakati wananchi watachoka manyanyaso na itakuwa vigumu kuwatuliza. Ni muhimu kuchukua tahadhari za mapema na kutafuta suluhu ya yanayoendelea kwa njia ya amani. Tuweke kipaumbele katika **kuifanya nchi yetu iwe salama na ya amani**. Ili hayo yaweze kutimia, **viongozi wetu watende haki kwani AMANI haiwezi kuwepo bila watu kupata HAKI. TUTENDE HAKI KABLA YA KUHUBIRI AMANI.**

Mungu Ibariki Afrika,
Mungu Ibariki Tanzania,
Mungu Wabariki Watanzania Wote.



JUMUIYA YA WANATAALUMA
UDASA
23 OCT 2025
S.L.P 35091
DSM
CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

Kwa niaba ya Jumuiya ya Wanataaluma wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDASA),

Imetolewa na

Elgidius Edgar Bwinabona Ichumbaki
Mwenyekiti wa UDASA
23 Oktoba 2025

JUMUIYA YA WANATAALUMA
UDASA
23 OCT 2025
S.L.P 35091
DSM
CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

Mtaa wa Uvumbuzi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, S.L.P. 35091, Dar es Salaam – Tanzania
*Simu*: **Mwenyekiti UDASA** +255 713 860875; **Katibu UDASA** +255 757 984 595
*Baruapepe*: ichumbaki@udsm.ac.tz; makukula.dominicus@udsm.ac.tz
Tufuatilie kupitia udasaudsm